# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS   TAMISEMI

Namba za Simu Mkuu wa Shule 0759359466

Makamu Mkuu wa Shule 0744261126

Mwalimu wa taaluma 0652474796

**SHULE YA SEKONDARI MAGADINI**

**S.L.P 41, SANYA JUU.**

Mzazi/Mlezi wa
Mwanafunzi ………………………..……………………………………………..

**MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MAGADINI WILAYA YA SIHA KWA MWAKA ………………….**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga  na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ………… na atasoma tahasusi ya **HGL/HGK**

**MAHALI SHULE ILIPO**

Basi unalosafiri nalo likiflka standi kuu ya Moshi mjini, Panda magari yanayoelekea Sanya juu kwa nauli ya shilingi Tsh. 3000/=. Ukitokea njia ya Arusha shuka kituo cha mabasi Bomang'ombe kisha panda gari la kuelekea Sanya Juu kwa shilingi 2000. Unapofika mwisho wa gari (Sanya juu) utapanda usafiri wa kukufikisha shule ya sekondari magadini Taxi shilingi 15,000/=, Pikipiki 4000/= na bajaji 8000/=.

**Muhula wa masomo utaanza tarehe………….mwezi wa……………………….mwaka hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……………mwezi wa……………mwaka  ………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………mwezi wa ………………..mwaka ………………….**

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:

2.1 Sare za Shule

| | |
|---|---|
| 1. | Sweta moja (kijani liliyo kolea) |
| 2. | Sketi mbili (kijani liliyo kolea)<br>Mshono: Rinda box moja kubwa mbele na moja kubwa nyuma isiwe na marinda mengine pembeni, urefu ufike kwenye kiwiko cha mguu. |

| | |
|---|---|
| 3. | Shati mbili nyeupe mikono mrefu |
| 4. | Gauni mbili za kushindia shuleni (Rangi damu ya mzee) mshono wa solo lifike karibu na kiwiko cha mguu.<br>Mwanafunzi haruhusiwi kuja na sare isiyo ya shule.. |
| 5. | Tai moja (kijani iliyokolea yenye mistari midogo myeupe) |
| 6. | Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi vyenye kamba, SOKSI ndefu nyeupe jozi 4,<br>Viatu viwe vya JUMA NA ROZA na visiwe na visiwe vya visigino virefu<br>Mwanafunzi pia aje na buti |
| 7. | Sketi rangi ya bluu (mshono solo) ya michezo ifike magotini,<br>T. shirt nyeupe na raba za michezo, |
| 8. | Track suit nzito yenye rangi nyeusi na mistari nyeupe pembeni (zisiwe za kubana) |
| 9. | Kwa wanafunzi wa kiislamu, shungi (hijab) nyeupe, ndefu inayopita kiwiko cha mkono |

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari saba counter books Q2 na daftari ndogo saba za mazoezi na begi la kubeba daftari.
ii. Rimu 2(A4) moja nyeupe isiyo na mistari (plain paper) ya pili iwe na mistari (rulled paper) kwa mwaka
iii. Scientific Calculator
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
    - Kwa wanafunzi wa HGL, waje na vitabu vya RIWAYA na Tamthiliya (An Enemy of the people by Henrick Ibsen, The Government Inspector by Nikolai V. Gogol, A test of Heaven by Farouk Topan, Animal Farm by George Orwell, Chasing the Leopard Finding the Lion by Julie Wakeman Linn, The opportunist Elite by Nyambari Nyangwine, The Horizon Unveiled by Fellowes Mwaisela pamoja na Vitabu vya History na Geography.
    - Kwa wanafunzi wa HGK, waje na vitabu vya Riwaya na Tamthiliya (Dunia uwanja wa fujo cha E. Kezilahabi, Ua la Faraja cha E. Mkufya, Mirathi ya Hatari cha C. Mung'ong'o, Wasifu wa Siti Bint Saad cha S. Robert, Mukwava wa Uhehe cha M. Mulokozi, Shujaa Mirambo cha E. Mbogo, Usaliti Mjini cha F. Imbuga pamoja na vitabu vya History na Geography.

v. Godoro linakodishwa shuleni kwa gharama ya Shilingi 10,000 kwa mwaka; AJE NA FEDHA TASLIMU.

vi. Chandarua

vii. Sanduku imara la chuma na kufuli

viii. BLANKETI MOJA NZITO

ix. Mashuka mawili ya rangi ya pinki

x. Mto na faronya za rangi ya pinki

xi. Nguo za ndani za kutosha

xii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

xiii. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

xiv. Paspoti moja ya rangi ya mwanafunzi (iliyopigwa karibuni)

VIFAA VYA USAFI

Mwanafunzi aje na brash ya chooni, hard broom, moper(squeezer), jembe na mpini.

Ndoo ndogo mbili (2), (moja kwa ajili ya usafi wa mazingira, ya pili ya matumizi binafsi ya wanafunzi)

Ndoo ya kudekia na dekio lake la mti.

Sabuni ya kusafisha vyoo lita tano (aina lemon multipurpose)

2.3 Michango mbalimbali

i. Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| i. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000 |
| ii. | Tahadhari | 5,000 |
| iii. | Nembo | 5,000 |
| iv. | Kitambulisho cha Shule | 5,000 |
| | Jumla | 80,000 |

NB. Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya **NMB 40101200098, SHULE YA SEKONDARI MAGADINI**

MATIBABU

Wanafunzi wanatakiwa na bima ya afya ya **NHIF**. Wanafuzi wasio na bima ya afya wanatakiwa kufika shuleni na kiasi cha shilingi 50,400/= ili waweze kukatiwa bima hiyo

Mwanafunzi mwenye tatizo kubwa la afya taarifa zitolewe mapema.

NB. Mzazi atagaramia nauli ya kwenda/kurudi hospitalini chakula pamoja na gharama za matibabu yasiyogaramiwa na bima ya afya.

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu Ia usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla nijambo lalazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation) iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakatiwote

ix. Kutunza mali za shule

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi

Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu

Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule

vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni

vii. Kufuga ndevu

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumiziya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba; xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi:

xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumbaza kulala wageni;

xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya
shule;

xv. Kudharau Bendera yaTaita;

xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

KARIBU SANA ………………

FELISTA Z KILEO

MKUU WA SHULE

NB:

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VYEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

i. Mkuu wa shule 0759359466

ii. Makamu Mkuu wa Shule 0744261126

iii. Mwandamizi Taaluma 0652474796

iv. Mwandamizi Malezi 0787667262

**THE PRESIDENT’S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

To be completed by a medical officer in respect of all form one and five students who join secondary school

**PART A**

TO THE MEDICAL OFFICER

……………………………….
STUDENT FULL NAME ………………………………………………………
Please examine the above named person as to be admitted to secondary school education

Signahtue .................... ……………. Designation..........................

Name of head of school……………………... ..Official stamp………………………

**PART B**: TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER

Blood count (white and red)…………………………………

Stool examination…………………………………

TB Test …………………………… Eye test ……………………….

Ears test…………………………….. Chest test……………………………….

Spleen test ………………………………….... Abdomen test …….. ...... pregnancy (girls only) …………………..

ADDITIONAL INT'ORMATION

Physical defect or impairment …………………………
Infection, chronic disease or family disease………………………………… . Othet information…………………………………………………..
Please citify that the above is fit to be enrolled at Magadini secondary school

Signature ………………….... Designation. ....................

Station………………………….. Date……………………………..

PART C: MEDICAL OFFICER CERTIFICATION

I have examined the above person and consider that she/ he is/not fit physically to join to secondary school.

Medical officer's name …………….

Signature………………..Date ……………………………Official stamp ……………..

HALMASHAURI YA WILAYA SIHA

SHULE YA SEKONDARI MAGADINI

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Mimi mwanafunzi .............................. mwenye umri wa miaka ………………. Jina kamili la baba ………………………….. Umri wa baba ni miaka…………………..
Wilaya..................... Tarafa
Kata…………..... Nambayasimu .................. Dini…………. Dhehebu la................. S.L.P
 ……………. Mimi mwanafunzi .................................... .ninakiri kukubaliana na kufuata sheria zote za shule.

Sahihi ya mwanafunzi ....................

Tarehe Mimi mzazi/mlezi wa ................................. ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shure.

Jina la mzazilmlezi ............................

Sahihi ………………………

Tarehe …………………………………………

| Picha yamzazi / mlezi | Picha ya ndugu wa karibu | Picha ya mzazi /mlezi |
|---|---|---|

Ndugu wa karibu aliyeidhinishwa na mzazilmlezi anayeweza kupewa taarifa au kuja kumtembelea mwanafunzi au kupewa taaifa za mwanafunzi endapo mzazi /mlezi hapatikani.

Jina kamili ……………………………

Uhusiano wake na mwanafunzi………………………....
namba ya simu …………………………….